

KPTJ
KENYANS FOR PEACE WITH TRUTH & JUSTICE

# Tuko Tayari au La?

## Maswala Kuhusu Awamu ya Pili ya Uchaguzi wa Urais

Makala ya kuongoza mjadala yaliyotayarishwa
na Erastus Wamugo

## Utangulizi

Tangu kurejeshwa kwa siasa za vyama vingi katika mwaka wa 1991, nchi ya Kenya imewahi kuwa na uchaguzi mkuu mara nne. Chaguzi hizi zimejumuisha uchaguzi wa urais. Isipokuwa katika uchaguzi wa mwaka wa 2002 ambao mgombea wa urais aliyeshinda alichaguliwa kwa kura nyingi zaidi ya 50%, chaguzi nyingine tatu zilishindwa kwa kiasi tu cha watu kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

### Ushindi wa watu wengi katika uchaguzi wa urais

| Uchaguzi wa | Mgao wa kura wa Mgombea Mshindi |
|---|---|
| 1992 | 36.4% |
| 1997 | 40.0% |
| 2002 | 61.3% |
| 2007 | 46.4% |



Asili: Tume ya Uchaguzi ya Kenya (ECK)

## Dibaji

Chapisho hili ni sehemu ya msururu wa makala ya mijadala juu ya uchaguzi mkuu ujao na unaotathmini matayarisho yaliyopo nchini kutekeleza uchaguzi ujao kwa njia ya amani na ya kuaminika huku ikiangazia na kutoa mapendekezo ya kupunguza hatari na matatizo yanayobainishwa. Uchanganuzi wa kina wa maswala halisi kuhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu ujao utachapishwa hivi karibuni.

### Vifupisho na Maneno ambatano

Tume ya Uchanguzi ya Kenya – ECK
Taasisi ya Mabadiliko ya Kidemokrasia – CDC
Tume Huru ya Ucahguzi na Mipaka – IEBC
Wakenya kwa ajili ya Amani kupitia Ukweli na Haki – KPTJ
Muunagano wa Kidemokrasia wa Kitaifa – NDC
Tume ya Uchaguzi ya Kitaifa – NEC
Chama cha New Patriotic Party – NPP
Upigaji kura wa awamu ya pili – TR
Mfumo wa upigaji kura wa awamu ya pili – TRS

Chaguzi hizi zote zilifanyika chini ya katiba ya zamani iliyokuwa na mfumo wa upigaji kura uliiyoruhusu ushindi kwa kiasi cha watu waliopungua 50%. Kama uchaguzi huu ungefanyika chini ya katiba mpya ya mwaka 2010, basi chaguzi zote tatu za –1992, 1997 na 2007, zingesababisha upigaji kura wa awamu ya pili.

Tangu uchaguzi wa urais uliopita, kura za maoni umefanywa na mashirika tofautitofauti kuhusu ruwaza ya upigaji kura katika uchaguzi wa urais. Katika chaguzi hizi, hakuna mgombea aliyeibuka na ushindi wa watu wengi zaidi ya 50%. Kwa hakika takwimu zilizofuatia kwa wagombea wanaoongoza kwa asilimia ya waliopiga kura hizo zimekuwa katika kiwango cha asilimia thelathini.

Kwa kuzingatia tajriba ya awali ya upigaji kura, ramani za kura za sasa na mabadiliko yaliyoletwa na katiba mpya, ukosefu wa utowajibikaji wa kisiasa pamoja na vyama vya kisiasa vilivyo hafifu, ni wazi kwamba kuna uwezekano wa kuwa na matokeo ya upigaji kura wa awamu ya pili katika uchaguzi ujao wa urais.

## Muhtasari kuhusu Mfumo wa Upigaji Kura wa Awamu Mbili

Mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili (TRS) unajikita katika msingi kwamba mgombeaji anapaswa kuungwa mkono na watu wengi zaidi katika eneo wakilishi alilochaguliwa.

Hali hii ya kuungwa mkono na watu wengi zaidi inasababishwa na matakwa ya usawa wa kidemokrasia. Kwa hivyo, mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili ni mkakati unaotumiwa kuafikia kuungwa mkono wa watu wengi kuliko ule wa awali ambapo mtu angeshinda hata akiungwa mkono na watu wachache katika uchaguzi. Mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili ni utaratibu sahili unaotokana na utaratibu wa upigaji kura wa awamu nyingi ambapo kila mara mgombea mwenye kura chache zaidi huondolewa. Utaratibu wa upigaji kura wa awamu nyingi ungali unatumika katika uchaguzi wa Baba Mtakatifu. Jamii za kisasa, hata hivyo, ni changamano zaidi na si kama baraza ndogo la siri la makadinali linalomchagua Baba Mtakatifu.

Mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili hutumika katika uchaguzi wa wabunge – mara nyingi katika Jumba la chini katika mfumo wa bunge mbili na katika uchaguzi wa urais. Katika uchaguzi wa urais, mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili hutekelezwa kwa wagombea wawili wanaoongoza kurudi kwenye kinyang'anyiro kwa mara ya pili ikiwa hamna mgombea aliyepata zaidi ya 50% ya kura katika uchaguzi wa awamu ya kwanza. Kuna tofauti katika mifumo ya uchaguzi kuhusu vizingiti vinavyoweza kusababisha upigaji kura wa awamu ya pili.

Pamoja na kwamba mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili unaendeleza thamani ya usawa, ubora wa mfumo huu unasemekana pia kujumuisha uendelezaji wa siasa za mapatano na ushirikiano, hivyo kuhimiza mwenendo ufaao katika siasa. Haja ya kuwa na miungano ya kisiasa inasemekana kuzalisha vyama na wanasiasa wanaojikita katika idadi ya wapiga kura na maeneo fulani mahsusi ya kijiografia.

Hata hivyo, uchaguzi wa awamu mbili una udhaifu na matatizo fulani. Udhaifu wa kwanza na ulio wazi kabisa unahusu gharama kubwa inayohusika. Pili ni uchovu unaoweza kutokea kwa wapiga kura wanapohitajika kupiga kura mara mbili. Kwa sababu hii, idadi ya wapiga kura katika awamu ya pili inaweza kuwa ya chini mno. Kwa kutoa ahadi nzuri kwa vyama mbalimbali ili kuungana na kuunga mkono chama fulani, mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili huondoa vitambulishi muhimu vya vyama na tofauti za kiitikadi ambazo hupatia vyama upekee. Katika muktadha wa Kenya mtindo huu una hatari halisi ya kushinikiza tofauti za kikabila kama msingi wa ushindani wa kisiasa.

## Tajriba ya Kenya katika Mfumo wa Upigaji kura wa Awamu Mbili

Mabadiliko ya katiba ya zamani ya mwaka wa 1988 yaliingiza mabadiliko katika sheria zinazoongoza uchaguzi wa urais. Kutokea hapo mgombea urais alihitajika kutimiza masharti matatu ya kisheria ili kutangazwa kuwa rais aliyechaguliwa. Mgombea urais alihitajika kupata kura nyingi zaidi katika uchaguzi wa urais, apate angalau 25% ya kura katika Mikoa isiyopungua 5 na mwisho awe amechaguliwa kama mbunge. Katika hali ambapo hakuna mgombea aliyetimiza masharti haya basi upigaji kura wa awamu ya pili ungefanyika baina ya wagombea wawili ambao wangekuwa na kura nyingi zaidi. Jambo la kustaajabisha ni kwamba matakwa ya katiba ya zamani yalihitaji kuwa mgombea atakayetangazwa mshindi katika awamu ya pili awe ametimiza masharti matatu ya awamu ya kwanza. Upekee huu wa uduara wa kikatiba haukuwahi kujaribiwa kwa kuwa katika chaguzi zote zilizotokea chini ya sheria hizi za uchaguzi, (1992, 1997 na 2002) mshindi aliibuka katika awamu ya kwanza. Katiba mpya ya 2010 ilileta mabadiliko mapya katika sehemu zinazohusu uchaguzi wa urais. Kwanza mamlaka yalibadilishwa kwa kiasi fulani. Kijiografia, mikoa yote – 8 kwa ujumla ilifutwa na maeneo mapya yanayoitwa kaunti – 47 kwa ujumla – yaliundwa.

Masharti mapya ya uchaguzi wa urais katika katiba hii mpya ni kama yafuatayo:
138 (4) Mgombea atatangazwa kama Rais akipata -
(a) zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa na
(b) angalau 25% ya kura zilizopigwa katika zaidi ya nusu ya kauti zote

Wakati ambapo hakuna mgombea aliyetimiza masharti haya, basi upigaji kura wa awamu ya pili utatekelezwa baada ya siku thelathini kutoka awamu ya kwanza. Uchaguzi huu wa awamu ya pili utakuwa kati ya wagombea wawili walioibuka na kura nyingi zaidi. Masharti hayo sharti yatimizwe na mgombea ili atangazwe kama mshindi.

Ikiwa sharti moja au yote mawili hayajatimizwa na mgombea mmoja, basi upigaji kura wa awamu ya pili utatekelezwa.

**Jedwali 1. Hali ya Uchaguzi**

| Je, mgombea ametimiza masharti haya mawili? | | | |
|---|---|---|---|
| | Asilimia 25% Sheria ya kaunti | zaidi ya asilimia 50% | Matokeo |
| Hali ya 1 | Ndio | Ndio | Rais aliyechaguliwa |
| Hali ya 2 | La | La | Awamu ya pili |
| Hali ya 3 | Ndio | La | Awamu ya pili |
| Hali ya 4 | La | Ndio | Awamu ya pili |

## Tajriba Linganishi

Mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili unajulikana sana katika mataifa yanayozungumza Kifaransa. Ufaransa yenyewe husemwa kuwa nchi yenye historia ndefu ya kutumia mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili. Hata hivyo, ni vyeme kuangazia mifano katika nchi za Kiafrika zinazozungumza Kiingereza. Hii ni kwa kuwa Kenya ina ulinganifu mkubwa nazo katika mfumo wa kisheria, asili ya sheria pamoja na pia katika asasi nyingine za kisiasa na hata utamanduni utamaduni.

### 1. Ghana

Wakati wa uchaguzi wa urais uliopita nchini Ghana, hakukuwa na mshindi dhahiri katika uchaguzi wa awamu ya kwanza uliotekelezwa tarehe 7 Disemba 2008. Mgombea katika tiketi ya chama tawala cha New Patriotic Party (NPP) alipata 49.13% ya kura huku mpinzani wake mkuu kwa tiketi ya National Democratic Congress (NDC) akipata 47.92% ya kura. Kura zilizosalia ziligawanyika miongoni mwa wagombea wengine sita.

Katika awamu ya pili, NPP kilipata 49.17% ya kura huku chama pinzani (NDC) kikipata ushindi wa 50.23%. Mbali na tofauti hii ndogo, matokeo yaliheshimiwa na wote na mgombea kwa tiketi ya chama pinzani alichukua hatamu za uongozi kwa amani. Pengine mazoea ya Ghana ya kutekeleza uchaguzi wa haki na kule kukosa umuhimu wa utambulisho wa kikabila katika siasa ni mambo yaliyochangia matokeo haya.

### 2. Liberia

Nchini Liberia, katika uchaguzi wa urais uliotekelezwa tarehe 11 Oktoba 2011, mgombea mkuu kwa tiketi ya chama tawala cha Unity Party alipata 43.9% ya kura huku mpinzani wake mkuu kutoka chama cha Congress for Democratic Change (CDC) akipata 32.7%. Kwa kuwa hakuna mgombea aliyeshinda kwa kura nyingi zaidi ya 50% kama inavyotakikana, upigaji kura wa awamu ya pili ulitekelezwa tarehe 8 Novemba mwaka huo. Kabla ya kutekeleza upigaji kura wa awamu ya pili, mgombea kwa chama cha CDC alijiondoa kwa uchaguzi huku akilalamikia udanganyifu kwa upande wa Tume ya Kitaifa ya Uchaguzi (NEC). Barua iliyotolewa na NEC iliarifu kwamba matokeo yalibatilishwa kati ya mgombea wa chama cha UP na CDC. NEC iliarifu waziwazi kwamba takwimu zilichapishwa kimakosa. Mwishowe, mkuu wa NEC alijiuzulu baada ya kumwachisha kazi mkuu wa mawasiliano. Ofisi ya Mwendesha mashtaka ilitoa taarifa ya onyo ikikanya dhidi ya vurugu. Hatimaye mgombea wa chama cha UP alishinda katika awamu ya pili kwa kuwa alikuwa mgombea wa pekee, lakini idadi ya wapiga kura ilipungua kwa karibu asilimia 50%. Hali ya nchi ya Liberia ingali shwari lakini bado haijulikani athari za kudumu zinazotokana na tukio hili zitakuwaje.

## Mashtaka ya Uchaguzi

Katiba mpya imeweka (na katika baadhi ya hali imeunda) mikakati pevu ya kushughulikia mashtaka ya uchaguzi. Kwa uchaguzi wa urais, Mahakama mpya ya Juu imepewa mamlaka ya kuamua uhalali wa uchaguzi wa urais. Hata hivyo, mamlaka haya, hutokea tu pale ambapo mgombea ametangazwa mshindi na tangazo hilo likazua utata kupitia mashtaka. Mamlaka haya hayagusii mashtaka yanayoweza kutokana na awamu ya kwanza wakati ambapo hakuna mshindi dhahiri. Mgombea mlalamishi amewachwa na nafasi ndogo sana ya kutafuta haki pamoja na muda mfupi sana kwa kuwa awamu ya pili sharti itekelezwa siku thelathini baada ya awamu ya kwanza. Kimya hiki na pengo katika sheria ni swala linalohitaji kushughulikiwa kwa dharura. Hali hizi zinazotazamiwa na masharti hayo mawili zimeratibishwa katika jedwali lifuatalo.

# Hitimisho na Mapendekezo

## Vyama vya Kisiasa

Sheria ya vyama vya kisiasa ya 2011, imebuni hali ya kudhibiti inayohimiza mielekeo miwili pinzani. Mwelekeo wa kwanza ni ule unaounga mkono kuwepo kwa chama huru cha kisiasa chenye katiba yake na pia matawi katika nchi nzima, kihifadhi usajili wa wanachama pamoja na kuwa sera na mipango yake. Ubora wa juhudi hizi ni kwamba chama kitazidi kushiriki katika shughuli za siasa kama vile uchaguzi. Muhimu zaidi ni kwamba vyama vina haki ya kupata fedha za umma kutoka hazina ya vyama kulingana na idadi ya viongozi wake waliochaguliwa. Mwelekeo wa pili unaohimizwa na sheria ni uundaji wa miungano na ushirikiano. Miungano inaweza kufanyika zaidi miongoni mwa vyama vidogovidogo ambavyo uhai wao unatishiwa. Hata hivyo, makubaliano ya miungano ni nyenzo bora ya kuhakikisha matumaini ya washirika katika uchaguzi pamoja na uwezo wa kufaa katika asasi za kisheria.

Je, utaratibu wa udhibiti utaathiri vipi mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili? Inawezekana kuwa vyama vitahisi kushinikizwa kuwa na wagombea wa urais (kupata mgao mkubwa katika hazina ya fedha za vyama) na kutumaini kupata miungano baada ya uchaguzi. Kuongezeka kwa idadi ya wagombea wa urais hasa wale wanaoweza kupata zaidi ya 5% ya kura kutasababisha kinyang'anyiro cha urais katika awamu ya pili. Kabla na baada ya uchaguzi, patakuwa na maafikiano yasiyo rasmi.

## Gharama za Kampeini

Mfumo wa upigaji kura wa awamu mbili una gharama ya juu siyo tu kwa serikali bali pia kwa vyama. Ni lazima wagombea wa urais watenge fedha kwa gharama zaidi ya kampeini na pia ni lazima Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ifanye hivyo pia. Sheria zinazobakia za kufadhili uchaguzi zinapaswa kuzingatia uwezekano huu wa kuwa na gharama zaidi katika uchaguzi wa urais.

## Elimu ya Umma na Uhamasishaji

Kuna umuhimu mkubwa wa kuwaelimisha wananchi kuhusu upigaji kura wa awamu mbili na kuwachangamsha kushiriki unapotokea. Hii ni kazi ya Tume Huru ya Uchaguzi ya Mipaka (IEBC) pamoja na wadau wengine katika mchakato wa uchaguzi. Wananchi pia wanapaswa kuelimishwa kuona miungano ya kisiasa kama ilivyo; kuwa ni utafutaji wa ushawishi wa kisiasa, na wala siyo 'usaliti'.

## Utulivu wa kisiasa

Katika tukio la awamu ya pili, muda baina ya awamu hizi mbili ni muhimu sana. Wagombea ambao hawaendi katika awamu ya pili wanafaa kukubali matokeo ya uchaguzi na kunapotokea utata, hali hiyo inapaswa kushughulikiwa kwa kina, kwa usawa na haraka iwezekanavyo. Awamu ya pili haifai kuangaliwa kama nafasi ya kuzua madhara. Hata hivyo, kuna hatari fulani. Sheria za kudhibiti vyombo vya habari zinapaswa kuwa zimewekwa wakati huu. Kwa hakika, iwapo uchapishaji wa kura ya maoni unapaswa kuruhusiwa katika kipindi hiki ni swala la mjadala.

Aidha, usawa katika serikali, mfumo unaotawala na asasi ni muhimu sana katika kuhakikisha utulivu wa kisiasa katika awamu ya pili.

KPTJ
KENYANS FOR PEACE WITH TRUTH & JUSTICE

KENYANS FOR PEACE WITH TRUTH & JUSTICE (KPTJ) is a coalition of citizens and organisations working in the human rights, governance and legal areas that came together after the crisis over the disputed results of the 2007 Presidential Election and the Violence that followed thereafter. Members include: Africa Centre for Open Governance (AfriCOG), Bunge la Mwananchi, Centre for the Development of Marginalised Communities (CEDMAC), Centre for Law and research International (CLARION), Centre for Multiparty Democracy (CMD), Centre for Rights, Education and Awareness for Women (CREAW), The Cradle - the Children's Foundation, Constitution and Reforms Education Consortium (CRECO), East African Law Society (EALS), Fahamu, FIDA-Kenya (Federation of Women lawyers), Foster National Cohesion (FONACON), Gay and Lesbian Coalition of Kenya (GALCK), Haki Focus, Hema la Katiba, Independent Medico-Legal Unity (IMLU), Innovative Lawyering, Institute for Education in Democracy (IED), International Commission of Jurists (ICJ-Kenya), International Centre for Policy and Conflict, Kenya Human Rights Commission (KHRC), Kenya Leadership Institute (KLI), Kenya National Commission on Human Rights (KNCHR), Kituo cha Sheria, Mazingira Institute, Muslim Human Rights Forum, The National Civil Society Congress, National Convention Executive Council (NCEC), RECESSPA, Release Political Prisoners Trust, Sankara Centre, Society for International Development (SID), The 4 Cs, Urgent Action Fund (UAF)-Africa, Youth Agenda.

A publication of the KENYANS FOR PEACE WITH TRUTH & JUSTICE. Reproduction is free with acknowledgement of KPTJ.

EDITORIAL, KPTJ, http://www.africog.org/kptj_homepage

KPTJ thanks Erastus Wamugo for allowing the publication of this paper in order to contribute to the knowledge and debate on elections under the new Constitution.

**Erastus Wamugo**
Governance Consultant
E-mail: erwamugo@yahoo.com